

1

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

### MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 28 Mwezi 02 2022.

#### KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MPANDA, S.L.P. 190,  
MPANDA ambacho kinawakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya  
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam ( ambacho katika mkataba huu atajulikana kama  
“Mwajiri”) kwa upande mmoja.

CORNER MAJINIO ALPHONSE S.L.P. NA 87, MBUGANI —

(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama “Fundi”) kwa upande mwininge.

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya  
CHUNYA;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje  
kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya CHUNYA;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya

UJENZI WA MFUNDO WA MAFUNDI  
KATIKA MAJENZO YOTE YA CHUO CHA  
UEIA CHUNYA.

**NA KWA KUWA** Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa  
vifaa vya Ujenzi (Schedule of materials) vinavyoonesha namna kazi itakavyofanyika;

**HIVYO BASI PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;**

#### 1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 12,252,000/-, Fundi  
atafanya kazi ya:

KUJENGA MFUNDO WA MAFUNDI KATIKA  
MAJENZO YOTE YA CHUO CHA UEIA CHUNYA

kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama “Gharama ya Ufundi”

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundu;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundu;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundu;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundu;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundu.

## 4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 02 mwezi 03 2020 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 18 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

## 5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

MFUMO WA MAJI

- (a) Kujenga TAKA na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;

- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*)ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA  
MPANDA

Jina: JOSUA MABANE Saini:



Wadhifa: NKUU WA CHMO Tarehe:

02/03/2022

Principal

Mpanda Vocational Training Centre

P . O . Box 190  
Mpanda

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ERASMIUS ZUMBA Saini:



Wadhifa: MWALIMU Tarehe:

02/03/2022

#### IMESAINIWA NA FUNDI

Mbele ya

Jina: CORNELY .M. ALPHONSE Saini:

G M Chambu

Wadhifa: FUNDI MIKEU Tarehe:

02/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: FULLY - SI AFAMISA Saini:

J'S'A

Wadhifa: FUNDI MSAIDIZI Tarehe:

02/03/2020